

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam
Tarehe 18 februari 2006**

Waliohudhuria

David Ludago
Elaine Baker
Rashid Jokolo
John Maximillian
Juma Jongo
Siyenu Mohammed

Joseph Ngalowoka
Maurus Malikita
Mejah Mbuya
Selemani Almasi
Shaban Ally

Usajili

John Maximilian na Elaine Baker walitoa maendeleo ya mwenendo wa usajili.

Kamati

John Maximilian aliomba kutolewa kwenye nafasi ya mweka hazina na kubaki kama mjumbe wa kawaida kwasababu hana nafasi ya kutosha kwani ni mweka hazina katika kikundi kingine.

Juma Ally Jongo alipendekezwa kuchukua nafasi hiyo na hakuna aliyepinga.

David Lugado alipendekezwa kubaki kama mjumbe wa tano kwenye kamati na alikubalika bila pingamizi na waliokuwepo.

Saa za mkutano

Mapendekezo yalitafutwa kwa ajili ya muda mpya wa mkutano saa 9.30 alasiri. Ndugu Siyenu alipendekeza kuwa tujaribu muda huo wiki itakayopfuata ili kuangalia kama mahudhurio yatakuwa mazuri kuliko asubuhi.

Ilijadiliwa ikiwa tunahitaji kukutana kila wiki. Ilikubalika tuendeleo kukutana jumamosi kila wiki.

Ilikubalika kwamba Elaine Baker atatoa vipeperushi halisi vyenye nafasi wazi za muda na tarehe kwa wajume ili wavitoe nakala na kuvigawa kwa wengine.

Kazi

Ndugu Siyenu aliripoti kuwa ametoa nakala kumi za shindano la insha ya baiskeli kwa watoto na kuzigawanya kwa waalimu na watoto.

Ilikubalika kuwa vitambulisho vya wajumbe wa UWABA vitolewe. Ilipendekezwa kuwa kitambuliso si lazima kiwe cha uanachama, ila kama mjumbe anataka, atatakiwa kuchangia gharama za utengenezaji wake. Ilikubalika kuwa hii atasubiri ubunifu wa nembo kwanza

Ilikubalika kuwa UWABA iandae kitabu chenye orodha ya matukio ya madereva wasioheshimu haki za wapanda baiskeli ili kuwaripoti polisi.